



OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI KONDOA
JARIDA LA HALMASHAURI



Januari— Machi 2020

Pendekezo Ilani ya Uchaguzi 2020-2025 kuwanufaisha wafugaji Dodoma



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma Mhe. Godwin Mkanwa akimkagua mbuzi aliyechinjwa katika machinjio ya mnada wa Bicha wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi uliofanywa na kamati ya siasa Mkoa wa Dodoma hivi karibuni.

SERA YA UHARIRI

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondoa. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kuitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondoa zinaweza kunukuliwa ili mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI

Bodi ya Uhariri

Msoleni Dakawa

Sekela Mwasubila

Flora Kyaruzi

Mawasiliano

S.L.P 711 Kondo

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

Mitando ya Kijamii



www.kondoatc.go.tz



Kondo TC



Instagram

kondoatc2015



KondoTC



@KondoTC

Barua Pepe
td@kondoatc.go.tz



Msoleni Dakawa

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondo

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hadi siku ya leo na kumaliza salama utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kipindi cha robo ya tatu.

Pili naungana na watu wote Duniani kutoa pole kwa mataifa yaliyopoteza wananchi wake maelfu kwa maelfu kutokana na ugonjwa unaosababishwa na Virusi vya Corona na nitoe wito kwa wananchi wote ndani ya Halmashauri ya Mji wa Kondo kuendelea kuchukua tahadhari ili kuepuka kuambukizwa ugonjwa huo kwa kufuata ushauri unaotolewa na wataalam na hadi sasa Halmashauri yetu haina mgonjwa mwenye maambukizi hata mmoja.

Aidha niwashukuru wajumbe wa baraza la Waheshimiwa Madiwani kwa kupitisha bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na baadae kupitishwa na Kamati ya Bunge yenye jumla ya shilingi bilioni 17.1 ambapo mapato ya ndani ni shilingi bilioni 1.4 bila kuwasahau watumishi wote waloshiriki katika maandalizi ya bajeti hiyo.

Hata hivyo niwapongeze pia Waheshimiwa Madiwani, Wakuu wa Idara na watumishi wote wa Halmashauri kwa kufanikisha Halmashauri ya Mji kupata hati safi kwa ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2018/2019 ikiwa ni mwaka wa tatu mfululizo Halmashauri inapata hati safi naamini imewezezeka na kutokana na kufanya kazi kwa umoja na mshikamano.

Vilevile katika kipindi cha robo ya tatu Januari hadi Machi 2020 Halmashauri ya Mji imepokea fedha kiasi cha Shilingi 272,080,782.91 kwa ajili ya (Elimu bila malipo, EGPAF, IMA, BASKET FUND na UNICEF na kuifanya Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2019/2020 kupokea kiasi cha Shilingi 638,300,264.32 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 30.3 ya fedha za miradi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yenye jumla ya Shilingi 2,102,026,006.94. Hata hivyo kwa kipindi cha Julai hadi Machi Halmashauri kupitia mapato ya ndani imekusanya shilingi milioni 979,250,781.45 sawa na asilimia 67 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2019/2020 na kutoa shilingi milioni 93,675,000 ikiwa asilimia kumi ya makusanyo kwa ajili ya mikopo ya Vijana, Wanawake na walemavu

Mwisho Halmashauri ya Mji ipo katika mchakato wa kujenga Stendi katika Barabara Kuu ya Dodoma Arusha hivyo nawasuhu wananchi wote kutumia fursa ya kununua viwanja na kuwekeza katika viwanja vya biashara vinyouzwa kuzunguka eneo hilo ili kujiinua kiuchumi na kufikia lengo la kila Mtanzania kuwa na uchumi wa kati.

BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI



Mhe. Hamza Mafita
Mwenyekiti wa Halmashauri



Mhe. Edwin Sannda
Mbunge Kondoa Mjini



Mhe. Zainabu Haroub
M/Mwenyekiti wa Halmashauri



Mhe. Kipaya Mdachi
Diwani kata ya Chemchem



Mhe. Abushehe Mbuva
Diwani Kata ya Kingale



Mhe. Ally Modu
Diwani Kata ya Suruke



Mhe. Besela Maunga
Diwani V/M Kondoa Mjini



Mhe. Abeid Boki
Diwani Kata ya Bolisa



Mhe. Ramila Abeid
Diwani V/M Bolisa



Mhe. Issa Kambi
Diwani Kata ya Kilimani



Mhe. Ezekiel Afande
Diwani Kata ya Serya



Mhe. Salimu Maguo
Diwani Kata ya Kolo

Pendekezo Ilani ya Uchaguzi 2020-2025 kuwanufaisha wafugaji Dodoma

Kamati ya Siasa Mkoa wa Dodoma mani kwa kuifungasha vizuri kusema kuwa katika mradi wa doma imeliweka suala la na kupata soko la uhakika machinjio katika mnada wa kuongeza thamani mazao ya jambo ambalo litawafanya Bicha waloutembelea Konfifugo katika Ilani ya wafugaji wapate maendeleo doa Mji thamani ya fedha iliyotumika inaonekana na inaridhisha.

Uchaguzi 2020-2025 kutoka na kuiinua kiuchumi na na kuongezeka kwa ufgaji mkoani humo.



Kaimu Afisa Mifugo Halmashauri ya Mji Kondoa Dennis Moshi akisoma taarifa ya uboreshaji wa miundombinu katika mnada wa Bicha mbele ya kamati ya Siasa Mkoa wa Dodoma walipofanya ziara katika mnada huo.

Kauli hiyo ilitolewa na Aidha alimpongeza Mkuu wa Mwenyekiti wa Chama Cha Wilaya ya Kondoa Mhe. Mapinduzi Mkoa wa Dodoma Mhe. Godwin Mkanwa wakati usimamizi mzuri wa miradi ndani ya wilaya ya Kondoa na iliyotekelzeza katika Wilaya ya Kondoa.

"Tunapenda Dodoma vi-jengwe viwanda vikubwa vya nyama na ngozi ili ngozi zote zinazotokana na machinjio hizi basi ziweze kupata soko lake kwa kuwa na sisi ni wafugaji wakubwa katika mkoa," alisema Mhe. Mkanwa.

Aliongeza kuwa uwepo wa kiwanda kikubwa cha nyama kutasaidia kuiongezea tha-

Awali akisoma taarifa ya mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika mnada wa Bicha Kaimu Afisa Mifugo Dennis Moshi alisema kuwa mradi huo umejengwa na wadau wa maendeleo shirika la LIC ambao walitoa shilingi milioni 51 na Halmashauri kuchangia shilingi milioni 2.

"Mradi huu umelenga katika kuboresha mazingira ya kibashara ya mifugo, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuimarisha ulinzi wa mifugo ya wafanyabiashara wa mifugo katika mnada ikiwa ni pamoja na kusogea huduma kwa jamii inayozunguka kata za Halmashauri ya Mji na wilaya za jirani za Kondoa na Chemba," alisisitiza Bwana Dennis.



Mjumbe wa kamati kuu ya Chama Cha Mapinduzi na mlezi wa Mkoa wa Dodoma Bi. Leyla Ngozi akisalimiana na wanachama walijitokeza katika mnada wa Bicha.

Kamati ya siasa mkoa wa Dodoma ipo katika ziara ya kutembelea miradi ndani ya mkoa wa Dodoma na iliambatana na baadhi wajumbe wa kamati kuu toka taifa na mkoani ikiongozwa na mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota.

"Fanyeni kazi mjilettee maendeleo" - Mkurugenzi Kondoa Mji



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa akizungumza na wananchi wa kata ya Chemchem (hawapo pichani) katika kikao cha maendeleo ya kata.

Wananchi wa Mtaa wa Chemchem yenu lakini kwa kuwa makusanyo ni na ya kujitolea hivyo inatakiwa katika kata ya Chemchem Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa bapo fedha hizo ndizo zinasaidia yenu na mfike mbali na nakushauri kufanyakazi na kujiletea maendeleo katika kununua vitendeakazi vya Mwenyekiti kuwaachia watendaji na ya Mtaa huo kwani maendeleo ya ofisi sasa ili tupate mgao mkubwa wajumbe kushughulikia masuala ya Mtaa huo yataletwa na wananchi tuongeze kasi ya ukusanyaji wa fedha ili wewe ubaki kuwa wenyewe na serikali ikitekeleza mapato ili tufanye mambo makubwa msimamizi wa hawa wote, "alishauri zaidi," alisitisiza Mkurugenzi Da-Mhe. Mafita.

Hayo yalismwa na Mkurugenzi wa kawa.

Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Akiongea katika mukutano huo kuanza kujitegemea kama Halmashauri ya Mji hauri katika program ya kusaidia mtaa huo wa kusikiliza kero za wa Kondoa Mhe. Hamza Mafita ali-kaya maskini TASAF kuanzia wapongeza viongozi wa Mtaa kwa mapema mwezi Julai ambapo Hal-kuchaguliwa na kumshauri mashauri imetengewa zaidi ya karibuni.

"Maendeleo ya Kondoa yataletwa na wanakondoa wenyewe na maendeleo ni gharama yanahitaji kujitaa kuanzia ngazi ya mtaa hivyo mkae na viongozi wenu muone jinsi ya kuongeza vyanzo vya mapato ya mtaa ili muweze kufanya maendeleo makubwa katika mtaa wenu," alisema Mkurugenzi Dakawa.

Aliongeza kwa kuwashauri wananchi kushirikiana na viongozi wa Mtaa huo kwani kwa kufanya hivyo amani itapatikana na kupata maendeleo.

"Mapato yote yanaingia Halmashauri ila baadaye hugawanywa kwa mujibu wa Sheria na katika mgawanyo huo kuna asilimia 20 ambayo huwa inakuja katika mitaa



Wananchi wa Kata ya Chemchem wakifuatilia agenda za kikao

"Kazi mliyopewa viongozi ni ngumu

Aidha Mhe. Mafita alitoa taarifa ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji hauri katika program ya kusaidia mtaa huo wa kusikiliza kero za wa Kondoa Mhe. Hamza Mafita ali-kaya maskini TASAF kuanzia wapongeza viongozi wa Mtaa kwa mapema mwezi Julai ambapo Hal-kuchaguliwa na kumshauri mashauri imetengewa zaidi ya karibuni. Mwenyekiti wa Mtaa wa Chemchem shilingi bilioni 2 na kwasasa inarati-kuwapangia kazi za kufanya wajumbe na Halmashauri ya Wilaya ya be wa serikali ya Mtaa waliochaguli-Kondoa.

wa ili kuwaleta maendeleo wananchi wa Mtaa wa Chemchem.

Diwani wa Kata ya Chemchem Mhe. Kipaya Mdachi aliwashi viongozi na wananchi kuilinda amani na kupendana ikiwa ni pamoja na kuepuka majungu, zaidi washirikiane kufanya kazi kwa pamoja kwani hakuna binadamu aliyejamili.

Wakitoa kero zao katika nyakati tofauti wananchi wa mtaa huo waliiomba Serikali kuwasaidia kuwatengenezea barabara katika kiwango cha changarawe, kupata maji safi na salama na kuwekewa taa za barabarani katika eneo la barabara ya Magereza hadi Hospitali.

Wazazi, walezi wapewa wiki moja wanafunzi kidato cha kwanza 2020



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota akiongea wakati wa kikao cha wadau wa elimu ,kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Ndugu Msoleni Dakawa.

Wazazi na walezi wa wanafunzi wanafanya kazi zao vizuri na mato-waliochaguliwa kuijunga kidato cha kwanza mwaka 2020 na hawajarioti katika shule walizopangisha wamepewa wiki moja kuhakikisha wanafunzi hao wanarioti na kuanza masomo kabla ya kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Agizo hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota wakati wa kikao cha wadau wa Elimu kwa ajili ya kujadili mafanikio na changamoto za elimu katika Halmashauri Kilichofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kondoa Irangi hivi karibuni.

"Wazazi iko shida kwenu mwanafunzi haendi shule na haumuulizi anapaswa kupigwa fimbo au mwanafunzi mtoro anakuja kumchongea mwalimu kwa mzazi badala yake mzazi anakuja juu kwa mwalimu hii si sawa tuache kulea watoto kama mayai tutawaharibu,"alisema Mhe. Sezaria.

Aidha aliwataka Maafisa Elimu Kata kufanyakazi zao kwa weledi kwani baadhi yao wameonekana wazembe kwa kutotimiza majukumu yao hivyo ili kufuta dhana hiyo ni jukumu lao kujituma katika nafasi zao na kuwasihii kuacha kuwapakazia ubaya Maafisa Elimu kwani

Akiongea katika kikao hicho Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Wa Kondoa Mhe. Hamza Mafita alisema kuwa ili kuondokana na matatizo ya elimu katika Halmashauri ni kuanzisha Mfuko wa Elimu ambao utasaidia kupunguza changamoto zinazoikabili Elimu ambapo kila kata itapewa fedha kulingana na jinsi walivyochangia ili kutatua changamoto zinazowakabili.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa aliwashukuru wadau kwa kujitokeza kwa wingi na kutoa mawazo chanya kwa lengo la kuboresha elimu ya mtoto wa Kondoa kwani maendeleo ya Kondoa yataletwa na wote walioshiriki kikao na wenye dhamana ya kuwahudumia wana Kondoa.

"Pamoja na yote kuanzia sasa ni marufuku Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule kuitwa Wilayani mara kwa mara kwani kunawafanya washindwe kusimamia majukumu yao iwapo Idara ina maagizo wafutateni hukohuko mashulen ikiwa ni pamoja na walimu wote na viongozi kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni

za utumishi wa Umma na kusirikiana na viongozi, wazazi na wanafunzi wote ili kuinua elimu,"alioneza Mkurugenzi Dakawa.

Mmoja wa wadau kutoka Mtaa wa Hachwi ikiwa ni moja ya Shule zilizofanya vibaya Bw. Salim Bura alisema kuwa kwasasa wanajamii ya Hachwi wameamka na kuona umuhimu wa Elimu ambapo kwasasa wapo tayari kumpatia nyumba ya kuishi bila malipo Mwalimu atakayepangwa katika Shule Shikizi ya Kotumo na kuiomba Halmashauri kuwafikishia huduma muhimu ikiwemo maji na umeme.

Kikao cha wadau kimeketi ili kujadili mafanikio na changamoto za elimu katika Halmashauri ya Mji wa Kondoa na kilianza kwa kusoma taarifa za Idara za Elimu na maazimio ya vikao vya wadau wa Elimu katika ngazi ya kata na taarifa za Ofisi za Uthibithi Ubora wa Elimu, Chama Cha Walimu na Tume ya Watumishi wa Walimu na kilihudhuriwa na Waheshimiwa Madiwani,wadau wa Elimu, Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu, Maafisa Elimu Kata, viongozi wa dini na Wazee maarufu.

Washauriwa kutumia mikopo ya vijana ilivyokusudiwa

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondo Msoleni Dakawa amewashauri vijana wa kikundi cha Kondo Quality Gypsum wanaotarajia kupata mikopo kutoka Halmashauri kutumia fedha hizo kwa malengo waliyokusudia na sivinginevyo.

Ushauri huo aliutoa alipotembelea kikundi cha Kondo Quality Gypsum kinachotengeneza mikanda ya gypsum na mapambo yake kilichopo katika Mtaa wa Maji ya Shamba hivi karibuni.

"Natamani mkue na baada ya miiaka miwili muwe na kiwanda chenu wenyewe muongeze kipato na mwisho mtakua kiuchumi sababu ninauhakika soko matalipata watu wanajenga sana Kondo kwa sasa na pia msiishie hapa anzisheni pia uuzaaji wa vifaa vingine vya ujenzi," alisema Mkurugenzi Dakawa

Pia aliwasihii kuwa na nidhamu ya fedha kwa kuwa fedha watakazopewa zinahitaji marejesho na uaminifu wao ndio utakaowapelekea kupewa kiwango kikubwa zaidi cha mikopo awamu nyingine.

"Msitoe fedha kwa mtu yoyote akidai kuwa amewapigania kupata mikopo hizi fedha ni zenu zipo kisheria mztumie ziliyyokusudiwa ikitokea mtu kawadai fedha yoyote ile toeni taarifa hiyo ni rushwa na haitakiwi kabisa," alisisitiza Mkurugenzi Dakawa.

Mkurugenzi amefanya ziara ya kutembelea kikundi hicho chenye jumla ya wanachama 10 kujiridisha na kazi wanayoifanya ikiwa ni moja ya vikundi vilivyoomba kupatiwa mikopo wa vijana kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri na marejesho ya mikopo ya awali ambapo kwa robo ya pili kiasi cha shilingi milioni 46 zinatarajia kutolewa.



Mzee ambaye ni mlezi wa kikundi na aliyetoa eneo kwa ajili ya uzalishaji wa mikanda ya gypsum kwa kikundi hicho cha Kondo Quality Gypsum akitoa maelezo kwa Mkurugenzi wa Mji kuhusu eneo la kujenga karakana ya uzalishaji ambapo kwasasa wanatumia uani kwake.



Sehemu ya mikanda inayozalishwa na kikundi cha Kondo Quality Gypsum



Halmashauri ya Mji Kondoa kutoa chanjo zote kwa mifugo



Mkuu wa Idara ya Mifugo Bibi. Monica Kimario akivuta dawa ya chanjo tayari kwa kuanza zoezi la utoaji wa chanjo ya minyoo na chambavu

Idara ya Mifugo na Uvuvi Hal- Aidha aliwashauri wafugaji ku-
mashauri ya Mji Kondoa imej- panga kuendelea kutoa chanjo
ya magonjwa ya Mifugo kulin- leta mifugo yao yote waliyo
gana na kalenda ya chanjo ina- nayo ili kupata chanjo kwani
vyoonyesha kwa mwaka mzi- baadhi ya wafugaji huleta mifu-
go michache kupata chanjo na
kuficha mingine hali inayohata-
risha kutokea kwa magonjwa
kwa mifugo ambayo haitapata chanjo.

Hayo yalibainishwa na Afisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mji Bi. Monica Kimario wakati wa utoaji wa chanjo ya ugonjwa wa Kimeta na Chambavu kwa mifugo ya kata ya Kingale.

"Nawasihi sana wafugaji wa Kata ya Kingale washiriki katika zoezi hili kwa kuleta mifugo yao katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utoaji wa chanjo ili kudhibiti magonjwa yatakayotoke bila kufanya hivyo mifugo itashambuliwa na magonjwa hayo," alisema Bi. Monica.



Daktari wa Mifugo Kenneth Maunga akim-
choma sindano ya chanjo ng'ombe katika
kata ya Kingale

"Chanjo hii ni salama kabisa na inatolewa na wataalam wa mifugo na hakuna matatizo yoyote yaliyotolewa kwa maeneo ambayo chanjo imetolewa na nawasihi wafugaji kutumia wataalam wa mifugo katika matibabu ya mifugo yao ili kuepukana na kupewa chanjo isiyo sahihi na hatari kwa mifugo yao," alisitisiza Bi. Monica.

Hata hivyo alitaja faida za mifugo kupatiwa chanjo kuwa ni pamoja na kudhibiti magonjwa, kuongeza uwezo wa wanyama kujikinga na maradhi, kupunguza gharama za matibabu na kuzuia magonjwa ya kuambukiza kutoka kwa wanyama kwendwa kwa binadamu.

"Hasara za kutopata chanjo nazo zipo ambazo ni kupoteza mifugo kwa vifo, kupunguza uzalishaji wa mifugo na uambukizaji wa magonjwa ya mifugo kutoka kwa wanyama kwendwa kwa binadamu," alibainisha Bi. Monica.

Halmashauri ya Mji Kondoa imejipanga kuhakikisha wanapunguza vifo ya mifugo na kuongeza uzalishaji kwa kutoa chanjo ambapo kwasasa imeanza kutolewa katika kata ya Kingale kwa magonjwa ya Kimeta na Chambavu ambapo kwa Halmashauri yote jumla ya ng'ombe 26,696, mbuzi 18,417 na kondoo 2782 wanatarajia kuchomwa chanjo hiyo.

'KCN' washauriwa kushirikiana



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa (wa nane kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wanaumoja wa Kondoa Community Networking mara baada ya kufungua mafunzo

Wanaumoja wa Kondoa Community kwao ndio kumewafanya wamefani-kuendeleza umoja walionao ili waendelee kui-marisha na kukuza malengo waliyojiwekea.

Ushauri huo ultolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa alipokuwa akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wanaumoja hao yaliyofanya katika ofisi za umoja huo Kondoa Mjini hivi karibuni.

"Umoja wenu ni chombo muhimu sana katikati Serikali ya awamu ya tano sababu mnasaidia katika kutangaza shughuli zinazofanywa na Serikali na kuwafikia wananchi moja kwa moja ikiwa ni pamoja na kujua dunia inavyokwenda," alisisitiza Mkurugenzi Dakawa.

Aidha aliwashukuru wajumbe wa umoja huo kwa kujitolea kwa hali na mali na kusema kuwa kujitoka



Wanaumoja wa KNC wakifuatilia mafunzo

inatambua kazi wanayoifanya hivyo washirikiane ili wafikie malengo.


"Umoja huu hautakiwi kuitwa Kondoa natamani ungeitwa National Networking kwa kuwa naona mpo

zaidi ya nchi moja nimesikia watu wa Egypt na Kenya hata njie ya mkoa wa Dodoma," alisema Mkurugenzi Dakawa.

Akiongea awali mlezi wa umoja huo Bw. Matogoro alisema kuwa kwasasa wamesimamisha kutoa huduma ya mtandao kutoptana na deni wanalodaiwa ambapo wanaendelea kufanya juhud za kutafuta fedha kupunguza deni hilo.

"Changamoto zingine zinazotukabili ni pamoja na sera kutotambua usajili wa umoja kama wa kwetu na uhaba wa maudhui ya kuweka sababu mengi yapo katika lugha ya kiingereza, lakini na-wapongeza Halmashauri ya Mji kwa kuweka maudhui mara kwa mara maudhui yao katika mitandao yao ya kijamii," alisema Bw. Matogoro

NAWA MIKONO KU-JIKINGA NA VIRUSI VYA CORONA



"Watendaji kusanyeni mapato" - Mkurugenzi Dakawa



Watendaji wa kata na mitaa Halmashauri ya Mji Kondoa wakimsikiliza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji (hayupo pichani) wakati wa kikao kazi katy yake na watendaji na baadhi ya Wakuu wa Idara.

Watendaji wa Kata na Mitaa waliofanya vizuri katika wao. wametakiwa kuhakikisha wana- ukusanyaji wa mapato kwa kusanya mapato katika maeneo mwezi Desemba na kumuagiza yao na kuwatolea taarifa watu Afisa Utumishi kumuandalia ki-wote wanaowakwamisha katika asi cha Shilingi laki moja Mtendaji wa Mtaa wa Kolo A Bi. Mary Baraka kutokana na kusanya mapato makubwa kuli-ko watendaji wote kwa mwezi Desemba.

Hayo yamesewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa wakati wa kikao cha kawaida cha uboreshaji utendaji kazi katy ya Mkurugenzi, Wakuu wa Idara na watendaji wa Kata na Mitaa kili-chofanyika katika ukumbi wa Chuo Cha Uuguzi Kondoa.

"Mkashirikiane na viongozi wa Serikali za Mitaa waliochaguliwa kuhakikisha mapato yanakusanya, nyie ni viongozi msome sheria mbalimbali zinazowaongoza na mzsirimamie na muachane na kutumia mashine za kukusanya mapato wanjie ya matumizi yaliyokusudiwa kwani kufanya hivyo ni kosa kubwa," alisema Mkurugenzi Dakawa.

Aidha aliwapongeza watendaji

"Kuweni wabunifu wa vyanzo nya mapato na muandae sheria ndogo za maeneo yenu kwani itawasaidia kuongeza mapato yatakayopelekea na nyie kupata gawio kubwa zaidi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zenu za kila siku," alisitiza Mkurugenzi Dakawa.

Aliendelea kuwasihii kuendelea kufanyakazi kwa kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni ikiwa ni pamoja na kufika kazini kwa wan-kati na kuheshimu kazi kwani wote watapimwa kwa kazi walizozifanya na kujiepusha kumiwa na watu wenye fedha kwani kwa kufanya hivyo watageuzwa kuwa watumwa

Akiongea katika kikao hicho Kaimu Afisa Elimu Bi. Anneta Narra aliwataka watendaji hao kushirikiana na viongozi walioteuliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kuijunga kidato cha kwanza wanaripoti shuleni na kuanza masomo.

"Mwamko wa wanafunzi waliochaguliwa kuijunga na kidato cha kwanza bado hauridhishi ni jukumu lenu kuhakikisha walipo majumbani wanafika shuleni ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wazazi umuhimu wa elimu na kuachana na mawazo ya kuwapeleka watoto wao nchini Oman kufanya kazi za ndani," alisitiza Mwalimu Narra

Hata hivyo Kaimu Afisa Mazingira aliwasitiza watendaji kusimamia shughuli za uzibuaijii mitaro hasa kipindi cha mvua, uchomaji wa mkaa maeneo ya makazi ya watu na usafi wa mwisho wa mwezi.

UJUMBE WA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA UNAOSABABISHWA NA VIRUSI VYA CORONA




HALMASHAURI
YA MJI KONDOOA

TAHADHARI YA VIRUSI VYA CORONA COVID-19

UGONJWA WA CORONA NI NINI?

NI AINA MOJAWAPO YA MAGONJWA YA MLIPUKO UNAOSABABISHWA NA VIRUSI JAMII YA CORONA (NOVEL CORONAL VIRUS 2019) NA UNASABABISHA HOMA KALI YA MAPAFU. KITAALAM UGONJWA HUU UNAITWA COVID-19.



DALILI ZA MTU MWENYE MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA



KUUMWA KICHWA



KIKHOZI



MAUMIVU YA MISULI NA
MWILI KUCHOKA



VIDONDAA KOONI



KUPUMUA KWA SHIDA

ENDAPO UNAHISI UNA MAAMBUKIZI AU UNAMUHISI YEYOTE PIGA SIMU KWA HARAKA KUPITIA 0762 069060
AU 0766 053243 NA WATAALAMU WA AFYA WATAFIKA ULIGO KWA AJILI YA KUKUSAFIRISHA.



www.kondoatc.go.tz



kondoatc2015



Kondoaa TC



HALMASHAURI
YA MJI KONDOOA

JINSI YA KUJIKINGA KUPATA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA COVID-19

MTU ANAWEZA KUJIKINGA KUPATA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA KWA KUFANYA YAFUATAYO



KUEPUKA KUSALIMIANA
KWA KUSHIKANA MIKONO



X
KUFUNIKA MDOMO NA PUA KWA KITAMBA
WAKATI WA KUKOHOA AU KUPIGA CHAFYA
AU TUMIA KIWIKO CHA MKONO



KUOSHA MIKONO MARA
KWA MARA KWA MAJI SAFI
NA SABUNI



KUEPUKA KUKAA ENEO LENYE
MSONGAMANO WA WATU

ENDAPO UNAHISI UNA MAAMBUKIZI AU UNAMUHISI YEYOTE PIGA SIMU KWA HARAKA KUPITIA 0762 069060 AU 0766
053243 NA WATAALAMU WA AFYA WATAFIKA ULIGO KWA AJILI YA KUKUSAFIRISHA.



www.kondoatc.go.tz




kondoatc2015



Kondoaa TC

WANANCHI MNA
TAKIWA KUEN-
DELEA KUCHUKUA
TAHADHALI YA KU-
JIKINGA KUPATA
MAAMBUKIZI YA VI-
RUSI VYA CORONA
KWA KUFUATA
USHAURI WA WA-
TAALAM WA AFYA.



MATUKIO KATIKA PICHA



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota akishauri jambo katika Kituo cha Afya Kingale baada ya ketembelea mradi huo



Mwalimu wa Shule Shikizi Msui akifundisha wanafunzi wa darasa la pili baada ya kujengewa shule hiyo na serikali



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Sezaria Makota akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa kuu na wataalam baada ya ketembelea mradi wa ujenzi wa jengo la Halmashauri



Viongozi wa Idara ya Elimu Sekondari wakiongea na wanafunzi wa kidato cha pili na nne katika Shule ya Mto Bubu



Afisa Mifugo akitoa risiti za kielektroniki wakati wa zoezi la chanjo ya Mifugo kata ya Kingale



Viongozi wa CCM Wilaya ya Kondoa wakikabidhiwa viwanja vine (4) walivyopewa na Halmashauri kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi ya makatibu wa Jumuiya ya chama.



HALMASHAURI YA
MJI KONDOA

TANGAZO LA UUZWAJI WA VIWANJA ENEO LINALOZUNGUKA STENDI MPYA YA MABASI NA MAGARI MAKUBWA BICHA



MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA HALMASHAURI INAUZA VIWANJA VYA BIASHARA KATIKA ENEO LINALOZUNGUKA STENDI MPYA BICHA ILIYOPO KATIKA BARABARA KUU YA DODOMA ARUSHA AMBAYO INATARAJIA KUANZA KUFANYAKAZI MUDA SI MREFU BAADA YA KUANZA KUJENGWA KWA MIUNDOMBINU YA AWALI KABLA YA KUANZA KUTUMIKA.

FOMU ZA MAOMBI ZINAPATIKANA OFISI YA ARDHI NYUMA YA BENKI YA NMB KWA SHILINGI ELFU 20,000 TU. KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA SIMU NAMBA **0716 956404** AU **0717 040 904**.

GHARAMA ZA VIWANJA NA MATUMIZI YAKE NI KAMA IFUATAVYO NA BEI HIZO NI KWA MITA MOJA YA MRABA.

NA	AINA YA KIWANJA	BEI KWA MITA MOJA YA MRABA
1.	COMMERCIAL PLOTS	4000
2.	FITNESS AND INDOOR GAMES	6000
3.	HOTEL	6000
4.	LODGE	6000

MATUKIO KATIKA BONANZA LA MICHEZO KATI YA WATUMISHI NA WANANCHI LILILOFANYIKA TAREHE 7/03/2020



Mshindi wa mchezo wa kukuna nazi Afisa Elimu Msingi



Mshindi wa mchezo wa kula alikula mikate miwili na soda tatu mwananchi



Washiriki wa shindano la kula pilipili na mshindi alikuwa mwananchi wa kwanza kutoka kulia alikula pililipi 10



Washindi wa mpira wa miguu timu ya wananchi wakipewa mbuzi wao baada ya kuwafunga watumishi goli 3-1



Wachezaji wa Timu ya watumishi kushoto na wachezaji wa timu ya wananchi kulia kabla ya kuanza mechi ambapo hadi mwisho wa mchezo watumishi wali-fungwa goli 3-1

